

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS,  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA MBOZI**



S. L. P. 3,  
MBOZI.

06/11/2023

Simu. Na. 025 – 2580272  
Nukushi Na. 025 – 2580044  
Baruapepe.ded@mbozidc.go.tz  
*Unapojibu tafadhali taja:*

**Kumb.Na. J10/MDC/5/13**

**TANGAZO KWA UMMA**

MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA MBOZI ANAPENDA KUWAJULISHA WANANCHI WOTE WA WILAYA YA MBOZI, MAKAMPUNI, MASHIRIKA, TAASISI PAMOJA NA WADAU MBALIMBALI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA MBOZI KWAMBA HALMASHAURI INATARAJIA KUHUISHA SHERIA ZAKE NDOGO ZA MWAKA 2015 PAMOJA NA MAREKEBISHO YAKE YA MWAKA 2018.

LENGO LA MABADILIKO HAYO NI KUTOKANA NA UHITAJI WA LAZIMA WA KUFANYA HIVYO BAADA YA SHERIA NDOGO ZILIZOPO KUPITWA NA WAKATI NA HAZIENDANI NA MAHITAJI YA SASA.

MATUMIZI MAPYA YA SHERIA NDOGO HIZO YANATARAJIA KUANZA RASMI MWEZI DISEMBA, 2023 KWA KUFANYA MABADILIKO KATIKA MAENEO YAFUATAYO:-

1. SHERIA NDOGO ZA UANZISHWAJI WA MFUKO WA AFYA YA JAMII
2. SHERIA NDOGO ZA ADA NA USHURU WA MAZAO, MASOKO, MINADA, MABANGO YA BIASHARA NA MAEGESHO.
3. SHERIA NDOGO ZA UTUNZAJI WA BARABARA ZA HALMASHAURI, MITAA NA VIJJI
4. SHERIA NDOGO ZA UANZISHAJI NA UTUNZAJI WA VYANZO VYA MAJI
5. SHERIA NDOGO ZA USAFI NA UDHIBITI WA TAKA
6. SHERIA NDOGO ZA MALIASILI NA HIFADHI YA MAZNIGIRA
7. SHERIA NDOGO ZA ADA NA USHURU WA MADINI
8. SHERIA NDOGO ZA ANUANI ZA MAKAZI NA POSTIKODI
9. SHERIA NDOGO (KANUNI ZA UKODISHAJI WA MITAMBO NA UZALISHAJI WA MATOFALI) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MBOZI.

HIVYO WANANCHI PAMOJA NA WADAU WOTE MNAKARIBISHWA KUTOA MAONI YENU KWA MUDA NA WAKATI UTAKAPOFIKA WA KUTOA MAONI YENU JUU YA RASIMU YA MABADILIKO YA SHERIA NDOGO HIZI KATIKA OFISI ZA KATA ZILIZOPO KATIKA MAENEO YETU YA HALMASHAURI YA WILAYA YA MBOZI..



*Abdallah H Nandonde*  
**MKUGENZI MTENDAJI (W)**  
**MBOZI.**

- NAKALA:**
- 1. KWENYE MBAO ZOTE ZA MATANGAZO.**
  - 2. OFISI ZA MAMLAKA YA VWAWA NA MLOWO.**
  - 3. OFISI ZA KATA NA VIJJI VYOTE.**
  - 4. TOVUTI YA HALMASHAURI YA WILAYA YA MBOZI**